

Zaidi ya dola milioni 28 zilizoidhinishwa kwa waathirika wa derecho huko Iowa

Release Date: Oktoba 28, 2020

Ime bakiya chini ya wiki moja kujiandikisha kwa usaidizi wa FEMA

DES MOINES, Iowa – Walio nusurika kwa derecho ya Agosti 10 wana chini ya wiki moja kuji andikisha kwa usaidizi wa janga na FEMA na kuomba mkopo wa maafa ya riba ndogo ya Amerika.

Hadi sasa, zaidi ya dola milioni 28 za msaada wa shirikisho zime idhinishwa kwa wakazi wa Iowa katika kaunti za Benton, Boone, Cedar, Clinton, Jasper, Linn, Marshall, Polk, Poweshiek, Scott, Story na Tama.

FEMA ime idhinisha zaidi ya dola milioni 9.7 katika misaada ya Msaada wa Mtu binafsi kwa zaidi ya kaya 2,640. Utawala wa Biashara Ndogo (SBA) ume idhinisha zaidi ya dola milioni 19 kwa mkopo wa majanga kwa wamiliki wa nyumba, wapangaji na wafanya biashara wadogo.

Maombi lazima yapokewe saa 11:59 jioni CST Jumatatu, Novemba 2, 2020, kuzingatiwa kwa msaada.

Habari ya usajili na maafa bado inapatikana kwa kupiga simu ya msaada ya FEMA, kwenda mkondoni au kutumia programu ya simu ya mobile ya FEMA, kwa njia zifuatazo:

- Nenda mtandaone kwenye DisasterAssistance.gov.
- Piga simu 800-621-3362 (TTY: 800-462-7585) kati ya saa 6 asubuhi na 10 jioni. Saa za Kati, (Central time) siku saba kwa wiki. Waendeshaji kazi wa lugha nyingi wanapatikana.
- Pakua App ya simu ya FEMA kwenye simu mahiri (smartphones).

Mwisho wa kipindi cha usajili haimaanishi FEMA inaondoka. Wakala utaendelea kufanya kazi na Jimbo la Iowa kusaidia manusura na jamii katika juhudi zao za kujenga na kupona kwa muda mrefu.



FEMA

Page 1 of 2

Mara tu uliposajiliwa, ni muhimu kuendelea kuwasiliana na FEMA kufuatilia programu yako au kuarifu wakala wa mabadiliko kwa barua zako za barua au anuwani yako ya email au nambari za simu, na kuripoti makazi ya bima, mahitaji yasiyo tekelezwa ya mahitaji au uharibifu wa ziada unaoweza kuwa nao

Wafanyikazi wa FEMA wanaweza kuwasiliana na wewe kwa sababu anuwai, pamoja na kujadili kesi yako au kuomba habari ya ziada. Jibu simu hizo ili kuhakikisha kuwa mchakato wako wa maombi unaendelea.

Ikiwa una shaka yoyote wakati unapokea simu kutoka kwa mtu anayesema anafanya kazi kwa FEMA, usitoe habari yoyote, lakini piga simu 800-621-3362 (TTY: 800-462-7585) kati ya saa 6 asubuhi na 10 jioni. CST kuthibitisha simu hiyo ni halali.

Wakati wazaki wa Iowa wanajiandikisha na FEMA, wanaweza kupelekwa kwa SBA. SBA husaidia biashara za ukubwa wote, mashirika binafsi ya faida, wamiliki wa nyumba na wapangaji. Msaada huu husaidia kwa matengenezo ambayo hayajalipwa au juhudi za kujenga upya na gharama ya kuchukua nafasi ya mali ya kibinafsi iliyo potea au iliyoharibiwa na majanga.

Kuomba mkopo wa maafa yenye riba ya chini kabla ya tarehe ya mwisho ya Novemba 2, kamilisha maombi mkondoni kwa disasterloan.sba.gov/ela/. Ili kufikia Mwakilishi wa Huduma ya Wateja wa SBA moja kwa moja piga simu 800-659-2955. Tuma maswali kwa njia ya email kwa FOCWAssistance@sba.gov. Kwa habari Zaidi tembelea sba.gov/disaster. For more information on the Iowa disaster and a variety of recovery resources, log on to: <https://disasterrecovery.iowa.gov/>



FEMA

Page 2 of 2